

OFISI YA RAISTAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

S.L.P 5616

TANGA

SIMU NAMBA: 0713398265

TAREHE.....

KUMB. NA MAPT SS/Join Ins/vol1/.....

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukupongeza na kukuarifu kuwa umechaguliwa kijiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mapatano. Shule itafunguliwa tarehe 11/1/2021 na mwisho wa kulipoti shulenii ni tarehe 28/2/2021.

Kikao cha wazazi/walezi kitafanyika tarehe 22/ 12/2021 saa 3:00 Asubuhi tafadhali uje na fomu hii siku ya kikao cha wazazi.

2. MAAGIZO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE ZA SHULE

i. **WASICHANA**

1. Sketi ndefu mbili (2) kitambaa aina ya Estem, sketi ya malinda ya kupanga
2. Mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya tomato
3. Soksi nyeupe ndefu.
4. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyo na kisigino kirefu.
5. Hijabu nyeupe ndefu

ii. **WAVULANA**

1. Suruali mbili aina ya Estem
2. Mashati mawili rangi nyeupe mikono mifupi (tomato)
3. Soksi nyeusi ndefu
4. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyo na kisigino kirefu.
5. Mkanda wa suruali mweusi usiwe na chuma.

NB: Bajaji haziruhusiwi, hijabu za suruali haziruhusiwi, mikanda ya suruali yenye chuma hairuhusiwi.

MAAGIZO MENGINE

Mwanafunzi aje na;

1. Madaftari kumi counter book (10).
2. Kalamu ya bluu na penseli.
3. Jembe lenye mpini.
4. Fagio la njiti la kufagilia.

5. Mkebe (Mathematical set).
6. Begi la kuwekea madaftari.

SHERIA ZA SHULE

Kwa mujibu w asheria ya Elimu ya Na. 25 ya mwaka 1978 imetoa sheria mbalimbali za shule ili kuleta nidhamu katika mazingira ya shule. Sheria zifuatazo zinaweza kukusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule, sheria hizo ni;

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi
5. Kupigana au kupiga
6. Kudharau bendera ya taifa
7. Kupata mimba/ kutoa mimba/kumpa mimba mwanafunzi wa kike.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kugoma, kuchochea ugomvi shulen au kushiriki kuvuluga amani na usalama wa shule.
10. Kukataa adhabu halali.
11. Kuwa na simu ya mkononi.

HITIMISHO

Mzazi/Mlezi zingatia maagizo yote yaliyotolewa katika fomu hii. Aidha hatutakaa shulen na mwanafunzi atakaekiuka taratibu zote zilizoelezwatika fomu hii. Tafadhalii mzazi/mlezi simamia jukumu la kusomesha mwanao kwa kumpatia mahitaji yote muhimu ya shule. Kwa mwanafunzi tii sheria zote za shule, tekeleza maagizo yote ya shule ili uweze kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na hatimaye kufaulu vizuri katika masomo yako.

Kwa maeleo zaidi au changamoto wasiliana na mkuu wa shule kwa namba tajwa hapo juu, tunakutakia maandalizi na utekelezaji mwema.

KARIBU SANA MAPATANO SEKONDARI

WAKO

.....

WANDI AM

MKUU WA SHULE